# MUHTASARI WA KIKAO CHA MKUTANO MKUU WA MWAKA (AGM)

**TAREHE:**15 February, 2026

**MAHALI:** UDASA

**Mahudhurio**

1. Japhet Masawe - Mwenyekiti
2. Matilda Kivelege – Katibu
3. Isdory Michael -Katibu Msaidizi
4. Magdalena Mbando -Mhazini
5. Hawa Liundi - Mjumbe
6. Tadei Kawa -Mjumbe
7. Herbert Temba -Mjumbe
8. Jerry Mjema -Mjumbe
9. John Mwenewanda -Mjumbe
10. Gladys Phares -Mjumbe
11. Dorwin Manyanja-Mjumbe

**Udhuru:**

1. Godwin Mwisomba
2. Deo Chale
3. Biseko Emmanuel
4. Ludovic Lukeha
5. Meshack Vitalis
6. Emmanuel Dominic
7. Zacharia Moshi
8. Gabriel Mruma
9. Ida Mrema
10. Lilian Wilson
11. Kurenje Mbura
12. Nelson Rwezaula

**Agenda**

1. **Ufunguzi**
   Kikao kilianza rasmi saa 9:10 alasiri kwa sala iliyoongozwa mjumbe.

2. **Utambulisho**

   Wajumbe waliofika walijitambulisha

3. **Kusoma ripoti ya historia na hali ya kikundi**

   Mwenyekiti alisoma ripoti na kuwashukuru wanachama ambao mpaka leo wameonyesha nia ya kuwa sehemu ya kikundi hiki. Kikundi hiki kilianza April 2024 kikiwa na wanachama 48, mpaka January 2026 wamebaki 43 ambayo mpaka Januari wamevuka lengo la kukusanya million 100 ndani ya miaka miwili. Lengo kuu ni kukusanya kiasi cha milioni 500 kwa kipindi cha 2026-2030 (Kiasi hiki kinaweza kuwa monetary or asset-wise).

4. **Kusoma ripoti ya fedha**

   Mhasibu alisoma ripoti ya fedha na kuainisha makusanyo, faini Pamoja na faida ya uwekezaji UTT. (Ripoti imetumwa kwenye group)

5. **Mapendekezo ya cha kufanya baada ya miaka miwili ya kukusanya mtaji.**
   Kwa sababu lengo la awali la kukusanya milioni 100 ndani ya miaka miwili limefikiwa, kikao hiki kilijikita kutazama nini au uwekezaji gani ufanyike baada ya kukusanya mtaji na kuutunisha.

   Yafuatayo ni mapendekezo ya nini kifanyike (NB: Mjadala huu ni kwa mujibu wa report ya fedha ya January,2026): -

✓ **Kuanzisha Muundo wa Mtaji na Hisa**

1. Maazimio:
   - Kwa makusanyo ya mpaka April 5, kila mwanakikundi atakuwa amechangia shiling 2.4mil. Na lengo letu la mil.500 maana yake hisa 10,000 zinaingia sokoni kwa thamani ya 50,000 kwa hisa.
   - Kwa muktadha huu, mpaka April 5, 2026 kila mwanachama atakuwa keshanunua hisa 48 au sote kwa jumla hisa 2064 (48*43)
   - Ili kufikia lengo tajwa la kukusanya mil. 500 (2026-2030), idadi 7936 zitakuwa sokoni kuanzia April 6, 2026.
   - Mwana kikundi anapaswa kununua aidha hisa 2 kwa kila mwezi (100,000) au zote 6 (300,000/=) ndani ya miezi mitatu. Ni lazima kila robo mwaka awe na minimum hisa 6.
   - Mwanakikundi mwenye uwezo wa kununua hisa zaidi ya 6 anaruhusiwa, iwapo tu jumla ya hisa zake zote hazitazidi 25% ya hisa zote.
   - Gawio kwa wanachama litategemea na wingi wa umiliki wa hisa hizi.
   - Kikao kilishauri iundwe kamati ili kuboresha hili wazo kwani linachochea ukuzanyaji wa mtaji kwa haraka.
   - Kamati hii itasimamiwa na kamati ya Fedha na Uwekezaji.

- ✓ **Kuanzishwa kwa Mfumo wa Kukopeshana**
    1. Maazimio:
        - Kikao kiliridhia 40% ya makusanyo yote ya miaka miwili itengwe na kuwa ya mikopo. Hii itafunguliwa sub-account ya UTT na itaendeshwa tofauti na account ya awali.
        - Kamati maalum ya mikopo kwa usimamizi wa kamati ya fedha na uwekezaji italeta mchanganuo wa kiasi na ukomo wa mikopo, muda pamoja na interests zake (Whole modality).
        - Mikopo yote itakatwa pesa (percent ya requested loan) kwa ajili ya bima kama kamati ya mikopo itakavyo shauri. Bima itawekezwa upya ili izae (sub-UTT account) na itatumika kufidia majanga ya mikopo.
        - Kamati hii itaundwa na watu watano, ambao watatu kati yao wanaweza Fanya maamuzi na yakapita kama ya kamati. Pia kamati haitahusisha wahasibu wala watia Saini.
        - Faida ya mikopo itaweza kugawanywa kwa wanachama kulingana na kamagawio.

- ✓ **Kuimarishwa kwa Uwekezaji wa Nje wa Kikundi**
    1. Maazimio:
        - Hili ndio lengo kuu la kikundi na 60% ya mtaji itabaki hapa.
        - Ikitokea fursa ya uwekezaji aidha kwenye hati fungani za muda mfupi au ardhi (kama kamati ya fedha na uwekezaji ilivyoshauri kwenye ripoti yao) mfuko huu utatumika kutekeleza uwekezaji huo.
        - Makusanyo ya 100,000/= kila mwezi yaliyoafikiwa kuendelea yanaingizwa mfuko huu.

**6. Katiba Mpya**

1. Maazimio:

- Uongozi uliainisha kuwa katika mazungumzo na awali ya mwanasheria ili kufanya marekebisho ya Katiba yaliyoainishwa kwenye kikao cha July, 2025.
- Kati ya kazi ambazo mwanasheria atatarajiwa kuzifanya ni Pamoja na: -
    - ✓ Kurekebisha Katiba yetu
    - ✓ Kuandaa na kufanya mchakato wa usajili ngazi ya LGA
    - ✓ Kuandaa fomu maalum za malipo ya waliotoka (To be expanded below)
    - ✓ Ni matarajio yetu Katiba kuwa tayari by 15th March, 2026.

**7. Haki mpya za wanakikundi**

1. Maazimio:
    - Baada ya miaka miwili, mwanachama atakayejitoa atarudishiwa 60% ya uwekezaji wake.
    - Pia Wanachama waliotolewa kwenye kikundi kulingana na katiba watarudishiwa pesa zao pamoja na faida (bila kiingilio). ***(Hata hivyo pendekezo hili litangoja ushauri wa mwanasheria)***
    - Hii ni sehemu ya kusawazisha mapengo yaliyo katika katiba iliyopo na kuzuia anticipated future legal problems.
    - Fomu maalum zitaandaliwa na mwanasheria ili kulifunga hili kisheria na kuzuia madhara ya mbeleni.

**8. Uchaguzi Mkuu**

1. Maazimio:
    - Kwa mujibu wa katiba yetu viongozi watakaa madarakani kwa miaka miwili
    - Kikao kimeridhia uchaguzi ufanyike tarehe **25/03/2026**
    - Uchaguzi utakuwa kwa njia ya mtandao (0NLINE).
    - Utaratibu na muda vitatolewa siku 7 kabla ya uchaguzi huo.
    - Ni matajio kuwa katiba itakuwa tayari kabla ya uchaguzi

**9. Kuanzisha Kadi ya Uanakikundi na Mfumo wa Taarifa za Wanakikundi**

1. Maazimio:
    - Kikao kiliamua kuanzisha simple kanzi-data yenye kuwa na taarifa muhimu za mwanachama kama NIDA, Mrithi/Mnufaika, namba ya uanachama
    - Kadi ya utambulisho zitaandaliwa

**10. Mengineyo**

Kikundi kinatarajiwa kufanya matumizi yafuatayo:

- Kulipa mwanasheria
- Ada ya kusajiliwa ngazi ya Halmashauri
- Kurejesha pesa za waliotolewa
- Kikao/AGM (188,000/=)
  ***NB: Gharama halisi za matumizi tajwa hapo juu zitawekwa kwenye ripoti za fedha kwa kadri zinapotumika.***

Kikao kilifungwa saa 1:15 usiku.